**Translator:** Maana yule aliyekua na ngombe akanyaganywa na yule aliye na kazi labda anapesa, anaenda kutoa pesa zake, anatafuta wakili na ananyanyasa yule mwingine asiye na uwezo wa kifedha.

**Kiptoon Cheserem:** *Basi konoe ne komwoe ole ndakotoretech bichu bo katiba atleast sityo kenyoru katorjinet.*

**Translator:** Kwa hivyo anawaomba enyi watu wanaohusika na Katiba kwamba mtuandikie hiyo ili ipate kutoka na baadye itusaidie tupate kuamua mambo.

**Kiptoon Cheserem:** *Agoi yoto che komoche amwa.*

**Translator:** Ni hayo tu niliyotaka niyaseme.

**Moses Bernard Lekumbe:** Majina yangu ni Moses Bernard Lekumbe. Na ninawashukuru sana kwa kuona ma-commissioners kwa kuweza kufika hapa ili kila mtu aweze kusema lolote lile anaonelea kulingana na maoni yale yanahitajika kwa Katiba hii ya Kenya sasa. Mimi maoni yangu nikikaa hivi, mimi naongelea kuhusu makabila yale ndogo kwa zingine. Na hayo ndiyo ninaongelea. Ikiwa Kenya sasa tunataka tu tuunde sheria ambayo inajali kila mtu. Kujali kila mtu ndiyo inalete amani. Kwa hivyo mimi ningeomba sana, na kwa upande wangu, ningeonelea kuna makabila madogo sana hapa Kenya. Na hao makabila, wengine hawatambuliki. Wengine kama vile sisi hapa Baringo tukiwa Jemsi. Sisi hatujulikana huku. Hata hatutambuliki ni kama sisi ni kabla ingine na infaa kwa serikali ile inakuja, iwe inajali masilahi ya watu wote. Inafaa iwe kila kabila ina Mbunge wao. Hii itamaliza tashushi ya kwamba, tumenyanyaswa. Sababu ikiwa ni kabla ile kubwa inatuongoza, hata ukitaka kwenda kuona hata Minister, au ukitaka kuona kama hata Mbunge, hakuna mahali utaonea, wewe ujulikani hata utambuliki, huonekani. Kwa lengo langu, ninaonelea hii mbuu ya katika hii sasa, iangalie sana. kila Mkenya ikiwa kabla ndogo, ikiwa kabla kubwa, ako na haki apate Mbunge anawakilisha kwa Bunge. Haijalishi area. Kuwe na Mbunge wa kuangalia masilahi yao kwa sababu - - kama watu wakiwa na shida, ndiyo haki inafikia. Yeye akilete reporti hiyo watu wanakubali isiwe inasemekana watu wale kwa vile Mbunge wangu ni jirani wangu sasa siwezi tosheka. Ikiwa mimi ni mtu wa wale wachache lazima nijaliwe hata mimi nijulikane Kenya. Mimi ni kabla fulani na niko-hata tukiwa wachache ni sawa.

Kwa hivyo, naomba kamati hii sasa ya Ma-commissioner, wale wanaandikisha, mchukue maanane kabisa ili kila kabila itambulike kwa Jamuhuri na ionekane. Na hata huduma ifikie hawa kwa njia ile iko sawa na wengine.

Nataka kugusia kitu kingine. Upande wa uchaguzi. Uchaguzi uwe kutoka councilor, mbunge, wachaguliwe na raia, na isiwe ati kwa vile yeye ako na masomo sana ati anapitishwa. Isemekane ni fulani tu atachaguliwa sababu yeye ako na masomo. Mtu yule raia watapenda, achaguliwe sababu huyu ndiye anajua shida ya raia wa area na ndiye unajua unaweza enda kwake. Kwa hivyo mimi ninasema pia Mbunge awe na ofisi mahali mtu anaweza mpata wakati wowote ukitaka. Hata akiwa hana wakati, mpaka kwa mwezi awe na siku nne. Mahali raia wanaweza mpata. Kwa sababu hii kazi ya Bunge mtu anachaguliwa. Anachaguliwa ni kama kumpatia mtu peremende na wewe unakula kitu chungu kama pilipili. Sababu hakujui. Anakujua wakati wa campaign. Wakati ulimchagua utamuona lakini wakati huo mwingine hakujui. Hata ukienda ofisi ofisi yake labda hata pengine ukiwa umefiwa, pengine mtu amechaguliwa hata minister, na unajua hiyo ofisi ni pahali fulani, unaenda unaambiwa “unamesa kitu gani?” Hataki kujua wewe, anasema mwambie hayuko. Kwa hivyo mimi ningetaka hawa wapunge wawe na ofisi mahali kamili.

Ndiyo, hata pia wameachilia kama councilor, wameachilia kazi kubwa na chief na Mkuu wa Tarafa. Sababu sasa hao ndio wanashugulika na hii mambo yetu kidogo kidogo kwa area. Na kuna ingine hata Mbunge angestahili na huna mahali ya kuona. Kwa hivyo yangu ningesema asante sana kwa kunipea nafasi hii. Asanteni.

**Com. Lenaola:** Willy Yator, halafu wanafunzi muwe tayari, Gladys Chelagat na Thadeus Kurere. Muwe tayari nitawaita baada ya Yator.

**Willy Yator:** Kwa majina ni Willy Yator. Nimeshukuru, yale nilikuwa nikitaka kuongea mengi yameongea. Yale nilikua nataka kuongea mengi yameongewa. Basi nilikuwa naoba kuongeza moja mwa upande wa matibabu, kwa hii Katiba tunaunda kwa sasa. Tungeomba Katiba itusiadie madawa yawe free kwa kila moja. Nikiongezea tena zaidi hapo ni kwamba Katiba kama vile iko kwa sasa, tuwe tukiwa kama Wakenya, iangaliwe isiwe ni Bunge, ndio wanarekebisha kila wakati. At least tuwe na wakati fulani maalum kama kiwangu ya tusema kama arobaini, ili tuanze kuangalia tena kurekebisha kosa lile liko katikati ama kile kingetaka kuongeza. Nafikiri kwa mengi yale nilikua nayo imesemwa nikaona hiyo tu ndiyo haijaguzwa.

**Com. Lenaola:** (Inaudible)

**Gladys Chelagat:** My names is Gladys Chelagat, I am in standard eight.

**Com. Lenaola:** How old are you?

**Gladys Chelagat:** I am fifteen years. Here are things we need to be helped in school. We need free education in primary schools, learning facilities, na tungependa michezo iendelee kama mwanzoni kwa shule. Kiboko iendelee ili watoto watilie maanane masomo. Tungependa watoto wasinyanyaswe wapewe chenye wanahitaji. Asanteni.

**Thadeus Kurere:** My names are Thadeus Kurere, I am 14 years old and I am in Standard eight. Here are things I am going to present. First of all as some have said we would like to have free education in Primary schools, e.g. donation of exercise books and text books because we have seen that every child leaves school due to lack of Primary School fees. The government has to help in order for us to proceed with our education because they pay for those who are in secondary schools and they don't pay for us.

Secondly, as it has been said, there should no withdrawal of the games because without the games it is very bad and even children can develop bad habits. Activities should go one e.g. games because we have to improve our talents. That is all I had.

**Com. Lenaola:** Thank you very much. Please go and register there. Thank you very much for your very eloquent views, we

thank you for coming. Isaac Chelagat? Afuatwe na Josephat Kipchirchir.

**Isaac Chelagat:** Jina ni Isaac arap Chelagat.

**Isaac Chelagat:** *Omwoe kongoi amu katiba ne kaitwech si kobit kenai tuguk che kimanai chi tai.*

**Translator:** Na shukuru kwa sababu ya mambo ya Katiba ambayo imetufikia ili tupate kuyajua mambo ambayo hatukuweza kuyajua hapo mbeleni.

**Isaac Chelagat:** *Eng tai kokikotom kenyoru uhuru ko kikiboisien kou ng'alekab chumbek ako chon che kikobou Kenya agoi raini makiguiye.*

**Translator:** Mambo ni kwamba kabla ya uhuru tulitawaliwa na mambo yaliokuwa yametengenezwa na wazungu na ilituongoza kabla ya uhuru mpaka wakati huu tulipopata uhuru tumekaa na hayo hayo.

**Isaac Chelagat:** *Ko nguno ko toretch katibaini mwanakenya si kobit kenyorun kiguyen kenai kiit ne tebtoi Kenya.*

**Translator:** Kwa hiyo Katiba hii ambayo sasa tunaiunda, itakuja kutusaidi sisi tukiwa wakaaji wa Kenya ili tupate kuelewa Kenya itakaa namna gani.

**Isaac Chelagat:** *Obwoti ole monomeikei kandoinateteb chumbek akoi chebo Africa anan ko Kenya.*

**Translator:** Uongozi wa Waafrika ama Kenya haitashikamana na ya wazungu.

**Isaac Chelagat:** *Basi ko mapendekezo omoche kesom katiba ketoben kimila nebo Kenya che kicham kotoretei.*

**Translator:** Basi pendekezo ni kwamba naomba kwamba mila ya watu wa Kenya iliyokua ikiwasaidia hapo mbeleni basi iangaliwe sasa.

**Isaac Chelagat:** *Amu kitinye kimila che toretei si ma chubisie chichi anan ko mayae kiy age tugul ne ya.*

**Translator:** Kulikuweco na mila iliyokua ikiongoza watu ili watu wasitukanane, ama ilikua ikiongoza watu wasipite mipaka.

**Isaac Chelagat:** *Kimoche nguno kigochi serikali kondena katiba si kobit kotebi kou noe si matokobitu bik che yoe atebwokik che yachen.*

**Translator:** Kwa hivyo tunaomba ya kwamba yale mambo yalikuweco mbeleni basi yarudi na ipate kukaa jinsi ilivyokua ikikaa hapo mbeleni.

**Isaac Chelagat:** *Si makinyonyosoni agot alak che nyalildos.*

**Translator:** Ili wale ambae ni walemavu ama wale ambao wanashida wasinyanyaswe.

**Isaac Chelagat:** *Basi obwoti ole kisome kou noe.*

**Translator:** Basi ni hayo tu naomba hivyo peke yake.

**Com. Lenaola:** Josephat Kipchirchir? Bada ya Josephat ni Miriam Chirchir.

**Josephat Kipchirchir:** My names are Josephat Kipchirchir Chepror. I am going to present in English. Now, in this commission, we thank our country for having prepared for us so that we can proceed on with our views. Now I have a view on our state of health as a nation. We have conditions which expose our people to ailments that are leading to disabilities. We have heard (inaudible) walemavu kama viziwi na viwete, the blind and all those who are affected physically and even mentally. We would like our country to eradicate things that can expose our people to such conditions. Like we have the loud music which is played in our matatus every now and then which can expose people to deafness. We hear of these cell phones that they contain a lot of radiation. Now this radiation also can expose our people to disability which will be a burdern ot our nation and even the people who are affected. We also have diseases like heart diseases which is as a result of various means. We have these cosmetics and our country should take note of those things which are imported from outside which contain  
and others which can expose our people to problems like kidney diseases which need a lot of money for treatment.

We now have diseases which need a lot of money for treatment. The country should plan, because we have been seeing our people on television on health plan who really suffer and they are exposed to be seen to be viewed every now and then, then the country can do something. If in our country we can contribute from the tax payers money. We have a lot of money which is got from the tax payers. Now, why can't the government do something because they are different cases which can be seen and they can be helped. I recommend that the government plans for our people's health.

Now, finally, the physically handicapped, mentally handicapped and even the deaf and the blind, they should prepare conditions which are necessary. Like for instance we have problems on those who want to get services like telephones and even in offices. The government has not done anything concerning these people, so we would like the government to take note and help them because these people are suffering. Thank you.

**Miriam Chirchir:** Kwa majina naitwa Miriam Chirchir. Pendekezo langu ningependa (inaudible) preschools. Pre-schools

should be considered first since it is the key to the formal education. Sana sana tukiangalia upande wa mama saa ile wanazaa, mtoto anaangaliwa sana, na hiyo maisha ni ya maana. Sasa watoto wakiachiliwa kwa Pre-school, na mtoto wangu nayeye ataingiaje kama hana masomo mzuri ama foundation mzuri?

Secondly, ninaongea mambo ya leadership kwa upande wa wamama. Sisi wamama tumesoma, tunaenda Beijing na tunataka uongozi wema, lakini hata tukiangalia sana sana concerning culture of the Africans, ama uongozi wowote katika kila nchi, wamama wanapaswa wawe mbele kwa uongozi. Sana sana sisi wamama tuko na shida sana na hatupaswi tuende mbele sana. Kwa upande wa Bibilia, hapo kulikua na uongozi sana, waliwekwa mbele wanaume, halafu sisi tukafuate. Kwa hivyo sisi hatuwezi-sitaki sana kusema ati sisi lazima tukuwe equal. We are not fighting for that equality, ati sisi tukuwe leaders mbele, ama kwa sababu sisi sasa tukuwe mbele kidogo. Hiyo iangaliwe.

On the side of leadership, ningependa sana kwa upande wa-tuseme mzee amepoteza bwanake na ingestahili mama ahakikishe apate title deed, halafu yeye mwenyewe ndiyo atagawia hao watoto wake ila sio watu wengine wakuje wagawiye hao watoto mali ya baba yao. Ikuwe ni mama mwenyewe anagawa mali kulingana na vile aliko na watoto wa huyo mzee wake. Tena, pia ningependekeza, the side of girls and boys should be equal. Kama ni dividing of the land, boys always should not be considered. Because ukiangalia sasa ratio ya girls and boys, girls wako wengi sana na hawa wasichana sasa unakuta wengi wanakosa bwana kuolewa sababu ratio yao ni nyingi, na inapaswa kama wewe ni mzazi, usione mbaya. Inastahili-the leaders should check on that na wakubalie ama walete hiyo mafundisho ya kwamba human right or any human being lazima apewe maisha yake mzuri. Iwe wewe umezaa wasichana, wapate maisha mazuri. Iwe ni kijana ni mtoto wako. It is your child.

Another one is on the side of agriculture. Sisi wakulima tunataka mazao yetu. Tunauziwa mbegu kali na baada ya kupata mazao tunauza bei rahisi. Bei inateremka lakini serikali inaendelea kuuza mbegu bei kali, na bei inateremka baada ya masaa. Sasa hiyo tuna-discourage sana wakulima. Sio mzuri. The government should check on that seriously, because ukienda kuangalia saa hii, ile kitu ya maana sana ni mimea ambayo inapatikana kwa shamba.

Last point, naongea kuhusu leaders. All leaders in Kenya, mtu akichaguliwa, tuseme awe nani au nani, you have been given any post. Ukiingia huko unaketi, siku ile unasikai kura inakaribia unakimbia sasa unaonekana kwa wananchi. Je, unajuaje shida za wananchi? Labda ni kitu tu unakwenda kulisha ndani yako. Sasa pendekezo lango ni kwamba mtu akichaguliwa, aende afanye ile kitu alipewa, aende akae kwa hiyo seat, sio kulala, kusaidia wananchi, asiwe akichaguliwa kwa . Ni hayo, asante.

**Com. Lenaola:** Thank you very much Miriam, I had asked for Joshua Chebatibin? Afuatwe na Alice Tarkok.

**Joshua Chebatibin:** Jina langu ni Joshua Chebatibin. Asante sana kwa commissioner. Nafikiri langu la kwanza nitasema kuhusu gender issue as regard to land inheritance. Tunaelewa katika jamii yetu wakati huu, kuna familia ingine ambayo labda

kuna watoto wengi na hawana shamba. Kuna wasichana na wavulana. Na katika jamii hiyo pia, wavulana wanaagaliwa zaidi kulikow wasichana. Ningependekeza Katiba mpya iangalie watoto kama ni sawa katika jamii, ili mzee agawie watoto wake shamba kulingana na vile anaona. Wasichana wasibaguliwe. Kuna hata jamii zingine ambazo zina wasichana peke yake na hawana wavulana naona jamii zingine yaani katika famili hiyo pia wanataka kunyaganya shamba ili kwa maana labda ndungu wa baba huyu, ana wavulana na ndugu yake peke yake. Wanakimbia nyumba ile ingine, wanachukua mashamba kwa sababu hawana wavulana. Kwa hiyo ningependekeza Katiba iangalie ili wasinyaganywe wapate haki zao.

Nitaharakisha sana. Jambo la pili ni kuhusu disabled. Walemavu katika jamiii waangaliwe na serikali pia ichunguze ili kuona njia ya kuwasaidia hawa kutoka national mpaka grassroot level. Wakisaidiwa na Ma-chiefs na Assistant Chiefs ili watambue ni wakina nani wanahitaji msaada. Na la tatu, ni kuhusu watu wakongwe katika jamii zetu za Kenya. Kuna wazee ambao wamezeeka pamoja na akina mama pia, na zamani walikua wakionekana wakiwa watu wa manufaa katika jamii, lakini ifikapo uzee wao, wanamaliza kwa njia mbaya sana. Wengine hawana watoto na wegine wanao. Ningependekeza pia serikali ama Katiba mpya ichunguze mambo haya ili kwamba wazee hawa wakongwe, wapewe idara fulani ambaye itawashugulikia kutoka the location ama sub-location mpaka Division na hata District ili wapate msaada kutoka serikali in the side of food, shelter and probably clothing. Ili wasimalize maisha yao kwa njia mbaya. Hata wengine wale ambao wana watoto, watakua katika nafasi ya kuangamia zaidi.

Jambo la nne ni kuhusu religious groups katika nchi hii yetu ya Kenya. Ningeomba pia hiyo groups ziwe minimized na hata wale ambao wangependa pia kuishi katika nchi yetu ya Kenya wa-register groups zingine mpya, wawe banned because we have had enough of these religious groups in Kenya so they should sieze.

Jambo lingine la tano, ni kuhusu rights of the child. Education should be free in our primary schools in order for all children to learn and have access to education, and also for the betterment of their future life, na along with that also health services should be free to everybody in Kenya especially at this time when we have had a lot of serious diseases which cannot be cured easily and also, kuna jamii zingine pia amabazo tukiangalia kuna watoto ambao hawawezi kujimudu hata kula chakula katika nyumbani ama katika jamii zao. Kwa maana there is no food, maybe the family has go no land and they are always out to look for food. I am also requesting for the new Constitution to look into that issue so that these children are also catred for, or a law should be enacted so that these people are looked into.

Jambo la sita ni illegitimacy in our society. Presently in Kenya, ningeomba pia Katiba mpya iangalie ili kwamba wanawake ama wasichana-mothers should not have children who do not belong to anybody.

**Com. Lenaola:** (interjections)

**Joshua Chebatibin:** I think we have because we are also having some street children who do not know their fathers, kwa

hivyo ningemba Katiba iangalie,

**Com. Lenaola:** (Inaudible)

**Joshua Chebatibin:** Kumetokea siku hizi, zamani hatukua nao.

**Com. Lenaola:** (Inaudible)

**Joshua Chebatibin:** Imetokea tabia fulani ambazo hatuwezi kujua sana, kwa hivyo ningemba serikali pia iangalie ili watoto wale wanapatikan wasiwe watu ambao hawana, they don't have anywhere. Kwa hivyo akina mama mjihadhari ili mjue mtoto ni wa nani.

Lastly, ni basic family needs. Each member of a family should be productive in every family in order to avoid this case of poverty and also utilize even the little land you have, so that your children cannot suffer. Thank you very much.

**Alice Tarkok:** *Eng kainet kegunon Alice Tarkok.*

**Translator:** Kwa majina ni Alice Tarkok.

**Alice Tarkok:** *Omoche ang'alale ng'alek ab lagok eng betusiechu.*

**Translator:** Nataka nionge juu ya watoto wa siku hizi.

**Alice Tarkok:** *Betusiechu kou werik ak tibik kolen werik acheng'chinikei kwondonyu kolen chepto acheng'chinikei murenenyu.*

**Translator:** Siku hizi wasichana wanasema wanajitafutia mume na kijana anasema anajitafutia mwanamke.

**Alice Tarkok:** *Ko amu cheng'chinikei, kosikchini lagok aeng koyonda amami chi ne teben amu kicheng'chinikei.*

**Translator:** Na kwa sababu alijitafutia peke yake anapatia huyu mtu watoto wawili kisha baada anamfukuza maana hakuna mtu alimuhusiha ila ni yeye peke yake alijitafutia.

**Alice Tarkok:** *Kolen eng katiba ni nyonei ko nyolu lagwa kwo koe anan koteb tie agoi kebwa koe asi kobit ye bitu ng'olyo, ko tinye akichek sigik kiy ne mwoe amu kibendi koe ak lagweng'wai.*

**Translator:** Kwa hivyo kwenye Katiba mpya inayokuja ianadikwe kwamba kijana akae mpaka siku ile atakapoenda na wazazi wake kutafuta msichana, ama msichana naye akae na wazazi wake mpaka siku ile vijana na wazazi wake wanakuja, maana akipeanwa na wazazi jambo linapotokea kuna watu wa kwenda kuhusika na hiyo.

**Alice Tarkok:** *Amu yeon werit ko yekilen kelenji kalyain lagwani we lagwani kole kiocheng'e kaon kou ye kiacheng'e.*

**Translator:** Kwa sababu kijana huyu anakaa na huyu mwanamke kufika katikati ya maisha mambo yaliomazito anafukuza na akiulizwa kwa nini ulimfukuza anasema peke yangu maana ni mimi peke yangu nilitafutat yeye.

**Alice Tarkok:** *Ko ye kitebe chepto kelenji kalyain lagwani ngenyo eng kot? Kole kiocheng'e ngaam tabut nyu amu kiocheng'e.*

**Translator:** Na msichana naye akiulizwa “mbona umeiacha nyumba yako na umekuja nyumbani?” anasema “Basi wacha nikule taabu yangu maana ni mimi peke yangu nilijitafutia tabu hiyo”.

**Alice Tarkok:** *Ko kaigai kinde maanani yoe si kobit konyoru akichek meng'et ne kararan.*

**Translator:** Kwa sababu hiyo, tuweke katika Katiba yetu ama tuweke nguvu kabisa ili nawao pia wapate maisha mazuri baadaye

**Alice Tarkok:** *kora omoche otesyi agobo chepyosoik che kikitun ago eng mwisho sine komaigochi Mungu koi. Ko iroti ile kikoi mi katikati kakoro chito kole mekoiei koon akorok kotun age. Ara onjini ng'o kilya ko manai kole maiei simabakotebto.*

**Translator:** Basi, neno lingine nataka nichangie, ni kuhusu wamama wale ambao wanaolewa kwa njia mzuri, lakini baada ya kukaa katika nyumba zao kwa muda fulani pengine wasifanikiwe kupata watoto, baadaye wanafukuzwa kwa hivyo neno ni kwamba huyu mtu hastahili kumfukuza huyu na atafute maana kwa nini siku ile alipoenda kutafuta, hakuweza kufasili kujua kwamba atazaa ama hatazaa?

**Alice Tarkok:** *Ko machei kejalan agine masilahi chekwai amu melen ki magenyin.*

**Translator:** Kwa hivyo hata naye huyu, basi anastahili kufikiriwa ama kujaliwa kwa sababu haikua mapenzi yake akae vile amekaa.

**Alice Tarkok:** *Agoi yoe ngoberurok Jehova.*

**Translator:** Mpaka hapo tu, asanteni.

**Juma Kiplenge:** Good afternoon Honourable commissioners, it gives me great pleasure to make the following submissions on my own personal accord. I have agonized through this Constitutional review process as an individual and I wish to make a comment that how do we ensure that the product of the commission is going to be a solution to the problems that we tend them to be?

Now, under Section 3 of the Constitution, it says that this Constitution is the Constitution of the Republic of Kenya and shall have the force of law through out Kenya and subject to Section 47 if any other law is inconsistent to this Constitution, this Constitution shall prevail and other laws shall to the extent of the consistency before it.

Now, under Section 47, it provides that subject to this Section, Parliament may alter this Constitution. Now, the question comes as to how does the Constitutional Review Act which enables this process to start, how can it be legitimized in the present Constitution? Now, there is a danger here that after you finish your work, these bodies may get an opportunity to file Court Cases and declare that this work is unconstitutional. My view is that it is legitimate. It is legal because it was created

to an Act of Parliament but it is not Constitutional, so some of these bodies go to court after your work, your is likely to be declared as Constitutional by a Court of Law, because what Parliament should have done in the first instance, is to entrench this commission in the Constitution as is presently, so that it reads; that is Section 47 should have been amended to indicate that subject to this Section, Parliament may alter this Constitution and/or Parliament can enact a law in order to review it. Because my understanding is that presently you are reviewing this very Constitution but you are not reviewing it in a manner that the Constitution provides. What does it mean? It means the manner in which the present Constitution is been reviewed, is inconsistent to the provisions of Section 47 and therefore it is (inaudible).

**Com. Okoth-Ogendo:** You know, I don't want to engage into a Constitutional argument in this particular point, but what is happening is really quite simple. Parliament says "We need advice", and Parliament has set up an institution to give it advice. Technically when that advice is completed, Parliament will decide whether or not to accept it and at that point Parliament will comply with Section 47.

There is no such thing as a Constitutional way of reviewing the Constitution. O.K.? There is simply a method, you see Parliament didn't have to set up the commission but having set up the commission, what the commission is doing is making a recommendation to Parliament and that is why the procedure involves handing over the report to the Attorney General who then publishes it as a Bill in the normal manner as availed to alter the Constitution and having published that Particular Bill, the Attorney General will take it to Parliament and at that point, Section 47 will be applicable, to if anybody goes to court and says

that this process is unconstitutional any sensible Court should say, “wait let us see if Section 47 will be violated” then say that the advice that Parliament is asking for is unconstitutional. There is nothing in the Kenya Constitution that stops Parliament from enacting legislation to enable it to receive advice from anybody else.

**Com. Lenaola:** For having so said, Juma please proceed and give your views.

**Juma Kiplenge:** I will leave that one to the test of time. Now, number two, I think personally that the mood of the nation is not right to accommodate this very process. The time that is allocated is very short and you will realize that most of the people who were coming here were sort of presenting their views with limited time. Now, in my view, Constitutional process is a long process of harnessing the spirit of the people. Now, in order to achieve a harvesting of the spirit of the people, in the problems which they present, it must be given adequate time.

Now, most people, most Kenyans reside in the rural areas, 90%. Most of them have never seen the Constitution. It was imperative that this document be translated into a language that people understood before asking them to give views for purposes of review. The record will bare me right that most of the issues that people address, of course at the end of the day it relates to the spirit in which they want a Constitution that protects or solves the same problem.

**Com. Lenaola:** (Interjection) I think you should leave what we have heard in other places to us. Please say what you thing about your own issues. Leave the commission to do its work.

**Com. Okoth-Ogendo:** And I think for the record Mr. Kiplenge, since 1990, there has been in excess of 45 Constitutions made throughout Africa. Non of them has taken a process as comprehensive as this one, infact what we are doing in this country is extremely unusual. Constitutions are not made this way. They are made over-night, they are imposed and they last-you know the shell life of an African Constitution is five years. So infact what we are doing, there maybe defect in what we are doing, but I think this country has got it right. We have at least gone to the people, but I think what we are here for is to hear your views about it rather than to argue as to whether or not it should have taken place, but let me assure you that there isn't anywhere that you are going to find a Constitution that is made in this kind of process. Nobody makes a Constitution like this. O.K.? They are made by the government, they are imposed, they are thrown out, whatever it is. We at least gave Kenya the credit of trying to go to the people if nothing else.

**Com. Lenaola:** And just to add that the nearest process to this, is South Africa, which was far far below the standards that Kenya has reached. So please give us your views however defective you think the process is.

**Juma Kiplenge:** I think, as I said these are my own personal views. I respect your views and these are my own personal views. Now, the last aspect of my submission. My argument is that the timing is short and been short, I urge that the electoral

process be delinked to this work that you are doing. You are doing a great job, which must not be hurried up for purposes of election.

Now, assuming that the commission presents a collected draft to the Attorney General, and the subject of debate does not end up in the desired way, there will be a Constitutional crisis because if we adjourn elections so that the document is ready and then the document takes along time before it is ready, it means if we adjourn the current elections timetable, it may never be held if there will be a problem on the product which you have produced and therefore it will create a President who might not be very good for the country, so my personal view is that-having argued that the time allocated is short, you should be left to finish your work, let the current elections be done on the time scale so that we are sure if any disagreement arises, it will not affect elections in any way whatsoever and also it will avoid a situation where it will create a bad President for other people to sort of take advantage. So those are my submissions, I have prepared a draft that soon after going through I will present it formally. Thank you very much.

**Com. Lenaola:** Thank you Wakili for your views. Kimwohoch Chemoiwo?

**Kimwohoch Chemoiwo:** *Eng kainenyu kegunon Kimwohoch Chemoiwo.*

**Translator:** Majina yake ni Kimwohoch Chemoiwo

**Kimochoch Chemoiwo:** *Omwoe kongoi missing amu amu kanyoru nafasi ang'alal eng kuhusu katiba ini.*

**Translator:** Ninashukuru kwamba nimepata nafasi ya kuchangia Katiba hii.

**Kimwohoch Chemoiwo:** *Basi ko netai ko komoche agobo kiruogik che iruogchini bik.*

**Translator:** La kwanza kabisa ni kwamba nataka nizingumuze juu ya Ma-chief ambao wanafanya kazi miongoni mwa watu.

**Kimwohoch Chemoiwo:** *Ko komoche ole eng waletab katiba keboibochini achek boisiek eng kiruogik kekwei eng gaa.*

**Translator:** Na kwenye Katiba hii ambayo inakuja ni kwamba sisi tunafurahia na tunapenda kwamba Ma-chief wawe wakifanyiwa interview na wazee nyumbani.

**Kimwohoch Chemoiwo:** *Basi ko kekwe anyun kekwe che somoniotin kong'ete Form Four agotestai.*

**Translator:** Na pia tuna unga mkono kwamba wakati wa kufanya uchaguzi tunachagua watu ambao ni wa kidato cha mne na kwenda mbele.

**Kimwohoch Chemoiwo:** *Amu eng yaet ab interview ko maya sine yakai lakini kikegeer achek kele tebyei kot komanda lagwet age ne tinye somanet akine ako yeitu anyun konyo kobichiit eng gaa moribei boisek ak lagok ak murenik eng gaa ak kiagik.*

**Translator:** Hatukatai interview hata wale ambao wamekuwa wamefanya lakini tumeshuhudia kwamba wakati mwingine inafanywa na baada ya huyu mtu kupita, akirudi nyumbani yeye aandamani na watu na wala hawezi akalinda watu wote ama masilahi ya watu wote.

**Kimwohoch Chemoiwo:** *Basi kechome kekwei eng gaa si kapkorok ..... amu ine koboisiwech eng gaa yekai tugul.*

**Translator:** Basi kwa hivyo tunapenda tuchague yeye hapa nyumbani maana yeye ndiye mtumishi wetu hapa nyumbani.

**Kimwohoch Chemoiwo:** *Basi ko komoche amwa eng waletab katiba ini eng chamaisiek che tawalani kou Kenya.*

**Translator:** Na pia nataka niongezee nizungumuze juu ya vyama ambazo zinapatikana hapa nchini Kenya,

**Kimwohoch Chemoiwo:** *Basi ko kochome missing ole tara yu boisie bichoe ko tara maichokosoni chamait age chamait age.*

**Translator:** Kwa hivyo naomba kwamba vyama hivyo vyote ambavyo vinapatikana katika nchi, zisiwe zikichokozana wao kwa wao.

**Kimwohoch Chemoiwo:** *Kaigai korib chi tugul chamainyi ak kosom chi tugul ng'echerenyi kou ye nyolunot eng mutyonet.*

**Translator:** Hivyo basi tunatoa pendekezo kwamba kila mtu atunze chama chake na aombe chochote anacho omba kwa njia ya upole.

**Kimwohoch Chemoiwo:** *Ago ye kitur age ko melen konerech is kobois ak noe kakaturis*

**Translator:** Basi na mwingine akishindwa asikasirike mbali apate kujiungana pamoja na yule aliyeshinda na wapate kufanya kazi pamoja.

**Kimwohoch Chemoiwo:** *Ak kesome anyun eng chamait ne mokoi koturis ko tara boisiewech eng oret ne kararan mokimoche tumdaet ab korotik.*

**Translator:** Na basi tunaomba kwamba kile chama ambacho kitakacho shinda, basi tunaomba kwamba kipate kutulinda na tukae na amani maana hatutaki umwagikaji wa damu.

**Kimwohoch Chemoiwo:** *Ago mokimoche ukabila.*

**Translator:** Na wala hatutaki ubagusi wa ukabila.

**Kimwohoch Chemoiwo:** *Kimoche kandoinatet ne ituitos bororiet ab Kenya.*

**Translator:** Lakini tunataka uongozi unavyo unganisha mataifa yote ya Kenya.

**Kimwohoch Chemoiwo:** *Kongoi missing.*

**Translator:** Asante sana.

**Com. Lenaola:** Jiandikishe. Asante sana. Msemaji wetu wa mwisho ni Lerimoi Toroitich. Na yule mzee nafikiri ndiyo mzee zaidi afunge mkutano.

**Rerimoi Toroitich:** Mimi naitwa Rerimoi Toroitich Mengich. Na kama naitwa Lerimoi Toroitich, pengine kama mimi nitaongea kidogo mimi nitaanza kukosa kwa neno. Sasa, mimi nitaongea juu tu kidogo halafu niongee kilugha. Mimi naitwa Lerimoi Toroitich kama mimi nakuja hapa mimi nakuja kwa chama. (Changes to Ki-nandi Dialect).

**Rerimoi Toroitich:** *Ko nguno obwote yue yu ko kakibwa agobo katiba.*

**Translator:** Basi natumaini kwamba tuko mahali hapa kwa sababu ya Katiba.

**Rerimoi Toroitich:** *Ko ngokakibwa kebwa yu katiba ko kakibwa eng boiboiyet.*

**Translator:** Vile tumekuja mahali hapa juu ya Katiba, tumekuja kwa furaha.

**Rerimoi Toroitich:** Na sisi tunataka tuone pendekezo moja hapa Kenya. Hapa Mochongoi, kuna mashule, kuna mashamba, lakini mimi napendekeza neno moja. Hapa Mochongoi tuna watoto wa shule. Kuna neno moja lilitokea juzi, na sisi wazee wa Mochongoi tukakataa; eti mtoto hawezi kupigwa kwa shule.

**Com. Lenaola:** Basi wewe pendekeza.

**Lerimoi Toroitich:** Lazima watoto wapigwe! Ya pili, Tukiwa hapa Mochongoi, zamani hatukua tunaona wamama wakismama mbele ya wazee/Bwana. Kwa hivyo sisi tunakataa!

**Com. Lenaola:** Kwa hivyo ungependa nini? Asimame nyuma ya mzee ama mbele?

**Lerimoi Toroitich:** Mama yuko nyuma!

**Com. Lenaola:** Jambo la tatu

**Lerimoi Toroitich:** Ya tatu ni kama tulivyo Mochongoi hapa, kuna Ma-chief, Ma-Sub-Chief, na Ma-councilor. Sasa hawa wote hukaa karibu mwaka moja kabla kuitana mkutano na bado wanalipwa.

**Com. Lenaola:** Kwa hivyo ungependa mkutano sasa

**Lerimoi Toroitich:** Kwa hiyo lazima mtu aajiriwe ili achangeie na kukutana na wananchi.

**Com. Lenaola:** Jambo la mwisho?

**Lerimoi Toroitich:** *Ngemi* yu la mwisho, kama tuko hapa Mochongoi, tuombe Katiba hii tukutane salama na watu.

**Com. Lenaola:** Asante sana. Mwalimu you are very late. So each of you come and say your name, give us a very pressing point and go and register. So Chelimo, kuja useme jina, give us one pressing point then sit down.

**Samuel Chelimo :** Jina langu ni Samuel Chelimo. Yangu ningependa kusema ya kwamba hii mambo ya Constitution hapa niko na points kama mbili tatu. Haya, ningependelea kwamba katika Constitution ile tuko nayo sasa umri ya kuwa Rais inaanzia miaka thelathini na tano na hapa hatuko na limit, kama ni ngapi. Ningependekeza miaka (inaudible) times two.

Haya, pia kuna mambo ya contesting kuwa Rais. Ningependelea pia katika Constitution ya sasa, inasema ya kwamba mtu anatakiwa kuwa Rais kwa vipindi mbili, na hapo ningependekeza ya kwamba hata wenywe wana-contest wapewe chances mbili ili Kiongozi wapya wapatikane haraka sababu hii mambo ya kupea mtu chances nyingi atatumia ile pesa ako naye kunyanyasa mwingine.

Pia katika Jamuhuri hii yetu ya Kenya mambo ya problem ya squatters iko nyingi sana. Sasa ningependelea katika hii

Constitution ile itatengenezwa, mambo ya squatters inagaliwe ili kila moja wetu katika Jamuhuri hii ya Kenya awe na ardhi. Yangu ni hayo.

**Com. Lenaola:** Asante sana mwalimu. Register pale. Next, say your name and proceed.

**Stanely Sang:** Kwa majina naitwa Mr. Stanely Sang. Leo hii niko na maneno mawili –matatu ya kuasilisha. Ya kwanza lina husu maneno ya elimu. Katika elimu yetu ya Kenya, wanafunzi wanapewa kazi kubwa ambayo ikifikia mwisho wa miaka kwa kweli hawana kile ambacho wamekipata. Kwa hivyo kile ambacho wamekipata kwa hivyo kile ambacho napendekeza ni kwamba ili tufikie kuwa na viwanda for industrialization, ni sharti tulete specialization right from Primary School level tulete specialization.

Pili ni maneno ya Constituencies. Ninapendekeza kwamba kwa zile constituencies ambazo tuko nazo, 210, kama ingewezekana ni kwamba tungerejesha hadi 188 kwa sababu tangu zile zingine zilipoundwa, kumetokea maneno ya kutoelewana baina ya majamii. Mpaka sasa ambapo ninaongea, kuna maneno ambayo inaendelea, boundaries hazijapatikana..

Kisha la tatu na la mwisho ni kuhusu maneno ya Wabunge Wabunge kuingia Bunge tunahitaji tuwe na age limit. Isimikane kama ni kuingia mule, kuwe na miaka ngapi mpaka ngapi. Tusiwe kwamba-Katiba sasa hivi inatuambia ya kwamba kwa maneno ya presidency, ni miaka thelathini na tano. Mpaka wapi? Kwa hivyo mimi ninahitaji two terms. Ikiwa kwamba ni 35 and above, kwa ile miaka ako nayo, aongezewe ile kumi peke yake juu yake na hiyo iishie hapo.

**Musa Loomul:** *Atinye ng'alek aeng kityo che omoche amwa. Omoche amwa ng'alekab.....(interjection)..... Jina yangu ko Musa Loomul.*

**Translator:** Majina yake ni Musa Loomul

**Musa Loomul:** *Ko kito ne omwoe ko ng'alekab bik ak ng'alekab mbarenik.*

**Translator:** Nataka ni zungumuze juu ya watu na juu ya mashamba.

**Musa Loomul:** *Kokochesane bik bik alak che borei kou ngokaik ago mokiroti ole tonone iman.*

**Translator:** Tumeona watu wengine wanaua watu kama ndege ama kama kuku na hatuoni mahali haki inasimama.

**Musa Loomul:** *Koech karon kele chit konye borei chi kele mi gaa ago kikobet nakonye mito timdo.*

**Translator:** Baada ya siku chache tunasikia kwamba yule mtu aliyewa mtu amerudi ako nyumbani na yule aliyeuawa haonekani

tena.

**Musa Loomul:** *Amu kakoweku serikali chito matokocham kebar.*

**Translator:** Kwa sababu serikali wamemurudisha, hawakutaka huyo mtu auwawe ama afungwe.

**Musa Loomul:** *Ko kito ne kemoche ko neu no kibo tai ko chito ne kibar chito ko lazima koyakta metit ab chito.*

**Translator:** Basi hapo mbelini ni kwamba mtu akiua mtu lazima alipe kichwa cha mtu.

**Musa Loomul:** *Basi noe ne karo ole kikoek hasara kome chito nin akorok kwo nino kosob kogeny.*

**Translator:** Basi hiyo ndiyo ile kitu nimeona kama nimefanya hasara maana yule mwingine amekufa na huyu mwingine ni hai.

**Musa Loomul:** *basi ko chuit ab serikali, serikali ne kitonon ng'olyondono matikocham koyayak kou noe.*

**Translator:** Basi aliyekataza kwamba kichwa kwa kichwa ni serikali walikataa hiyo.

**Musa Loomul:** *Komoche chito no kibar chito ko lazima kome agine kome amu kime nino.*

**Translator:** Nataka yule mtu ambaye aliyewa mtu hata na yeye auawe.

**Musa Loomul:** *Ne rubei ko omoche ng'alekab rurotusiek ab mbarenik ko takenyoru tuguk che karurio ko mokingen ole kioldoen.*

**Translator:** Basi lingine ni kwamba tuaomba ya kwamba baada ya mazao yakiiva yakipatikana, hatujui mahali pa kuuzia.

**Musa Loomul:** *Kimoche factorit ne kioldochini tugukyok che kiyoe eng eunekyok agoi makataik ab kiyakiyok.*

**Translator:** Tunataka tutengewe ma-factory na mahali pa kuuzia vitu vyetu ambavyo tunazo hapa kwetu nyumbani.

**Musa Loomul:** *Kimoche yoe mi factorit kolekitit ne kimuchi kenai ole mito si kapkorok koibei chito tugukyik.*

**Translator:** Basi tunataka tujue mahali factory kama vile ya ngozi na mambo ingine iwe karibu, kila mtu anaweza elewa na apeleke vitu vyake mahali pale.

**Musa Loomul:** *Ko tuguk choto che okose oimenkei omoche agas anai ole tokyingei.*

**Translator:** Basi mambo haya mawili ni yale ambayo naomba kwamba ipate kusikika na sijui itaelekea wapi.

**Com. Lenaola:** Mzee Musa kuja hapa. Wewe ndiwe msemaji wetu wa mwisho lakini kwa vile bado tuko na muda, ni nani ambaye kama kuna jambo ambalo kama hasemi, hata lala leo? Kuna mtu ako na jambo? Hakuna tumeshukuru sana. Yaani kama husemi hutalala? Kuja sema? Jina na jambo moja sawa?

**Joshua Chepcheing:** Mimi ni Joshua Chepcheing. Mimi napenda serikali iangalie mali ya wananchi. Mali ya wananchi hailindwi vizuri.

**Com. Lenaola:** Ungependa nini?

**Joshua Chepcheing:** Ningependa serikali (inaudible) serikali ya usiku na mchana kwa sababu mwizi anaiba saa tatu na askari anakuja saa moja.

**Com. Lenaola:** Anaiba nini?

**Joshua Chepcheing:** Anaiba ng'ombe, kondoo na vitu nyingi hata kuku.

**Com. Lenaola:** Sawa sawa Asante. Sema jina, lako moja, umalize.

**William Ngetich:** Jina ni William Ngetich. Langu ni juu ya Wabunge na Ma-councillors ambao wanachaguliwa na raia. Nilikua nataka kusema kwamba kwa utaratibu wa uchaguzi ni kwamba wakati sheria inapotengenezwa ni kwamba wakati wa kuhesabu kura, ihesabiwe katika kila station ambayo ilikua inafanyiwa hiyo kazi na ku-record-iwa hapo hapo, ndiyo results zichukuliwe mahali inapofanyiwa.

Halafu ya pili, ni kwamba wale wote ambao wanataka kujitokeza wapigiwe kura kama kwa wacouncil, au kwa Wabunge, ni kwamba waachishwe kazi baada ya kuchaguliwa, sio waachishwe kazi kabla hajamaliza mambo ya uchaguzi. Asante.

**Com. Lenaola:** Kuna mwingine ambaye anataka kusema chochote? Hakuna. Tumeshukuru sana. Maoni yenu ni mazuri, tumefurahia kuwa hapa kwenu. Tutamuita Co-ordinator atufungie mkutano, kasha maombi halafu tunawatakia mema. Asante.

**Elijah Litangule:** Naomba Chairman wa 3C's aseme moja, mawili halafu nifunge.

**Daniel Rotich:** Commissioners, members of the public, school pupils, my names are Daniel Rotich. I take this opportunity to extend my appreciation to all of you, who have actually taken your time to come and tell your views to these members of the

Commission. Commissioners, on behalf of people of Mochongoi, extend my appreciation to you all. And now I hand over to my District Co-ordinator, Mr. Letangule to take over.

**Elijah Litangule:** Mimi sina mengi ya kusema, kwa jina of course ni Elijah Litangule, Co-ordinator wa CKRC, Baringo District. Yangu kwamba ni kusema shukurani sana kwa nyinyi watu wa Mochongoi kujitolea kwa wingi, nafikiri hii ni station moja tumekua na watu wengi wamekuja kutoa maoni yao, na kwa hiyo na shukuru. Hata kwa upande wa civic education, ningependa kuambia Ma-commissioners kwamba Mochongoi ndiyo iliongoza kwa civic education. Vile vile ningependa Ma-commissioners wajue ya kwamba, Provincial Administration, Ma-chief wa hapa, bwana DO, Ma-councilor wamenipea support ya kutosha. Bila support yao nafikiri hatunge-mobilize vile tume-mobilize wakati huu.

Vile vile ningependa kushukuru providers wa civic education katika hii Division, sababu wameungana pamoja na viongozi na wamefundisha watu wetu kuliko mahali pengine pote Baringo District. Kwa hayo nasema asante sana kwa watu wa Mochongoi.

Kwa hivyo kwa sababu Ma-commissioners wamechoka sana, nafikiri nitampea nafasi mama ama mzee moja atufungie kwa maombi ili pia tuweze kufika manyumbani mapema kidogo. So, volunteer mmoja, Pastor? Ninaona kama yuko around.

**Elijah Cheruiyot:** Basi tusimame tukiomba maombi ya mwisho. Basi natuombe. Mtakatifu Mungu wa Binguni katika jina la Yesu, tunasimama mara tena mbele zako tukitoa shukurani mbele zako kwa sababu umekua pamoja nasi tangu wakati tulipoanza mkutano huu. Umekua mwaminifu kwa kuongoza kila moja, yale yote ambayo tumetoa katika vichwa vyetu tuataka tukushukuru maana umetuwezesha. Naomba ya kwamba baraka zako zipate kuandamana na kila moja wetu. Tunakushukuru kwa sababu ya afya zetu. Tuakushukuru kwa sababu ya usalama wetu, tunakushukuru kwa ajili ya nchi yetu, tunakushukuru kwa ajili ya viongozi wetu. Tazama wakati huu hata hawa wageni wetu ma-commissioners, watakapokua wakirudi katika shuguli nyingi walizonazo, nawaombea baraka zitokazo kwako Mbinguni, kwamba Mungu upate kuwapatia nguvu, hata na uwezo wa kuweza kuketi na kusililiza, kisha baadaye wapate kufanya kazi hiyo kwa moyo na mwishowe Mungu tutakua na jambo nzuri ambalo tutafurahia tukiwa wakaaji wa Kenya.

Bado tunakumbuka hata wazee na wakina mama na watoto. Kila moja aliyeweza kusimama na kutoa hoja zake. Mungu naomba baraka kwa ajili yao. Mungu wetu wakati huu tunapoelekea kumaliza na kuondoka, tunaomba baraka zako zipate kuandamana na kila moja wetu, maana tumejiwacha mikononi mwako, tukiamini ya kwamba usalama na ulinzi unaotoka kwako utakua ni wa milele, hata mwishowe Mungu utusaidie tupate kuelewa neno lako, hata mwishowe tupate kufika kwako Mbinguni, mahali umeenda kutuandalia. Nimekushukuru, niseme asanti kwa yote, maana nimeomba nikiamini umetusikia, na utaenda kututendea hivyo. Katika jina la Yesu Kristo, aliye Bwana na Mwokozi wa Maisha yetu, Amina.

Meeting ended at 3.05 p.m.

